

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI Z
MITAA



HALMASHAURI YA WILAYA YA USHETU

Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na. UDC/L.40/08/11

17 Agosti 2020

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu anawatangazia nafasi za kazi watanzania wote wenye sifa za kuajiriwa katika nafasi ya Mtendaji wa Kijiji III. Tangazo hili linatokana na Kibali cha Ajira mbadala kilichotolewa kwa barua yenye Kumb. Na: fa.170/376/01 "A"/08 ya tarehe 04 Agosti 2020, kutoka kwa Katibu Mkuu OR- Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

MTENDAJI WA KIJIKI DARAJA III – Nafasi 03.

SIFA ZA MWOMBAJI;

1. Awe amehitimu Kidato cha Nne (IV) au Sita (VI).
2. Awe amehitimu mafunzo katika ngazi ya Astashahada/Cheti katika moja ya fani zifuatazo; Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya Jamii, na Sayansi ya Sanaa kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo, Dodoma au Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

KAZI/ MAJUKUMU

1. Afisa Masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji;
2. Kusimamia Ulinzi na Usalama wa raia na mali zao, kuwa Mlinzi wa Amani na Msimamizi wa Utawala Bora katika Kijiji;
3. Kuratibu na kusimamia upangaji wa utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Kijiji;
4. Katibu wa Mikutano na Kamati zote za Halmashauri ya Kijiji;
5. Kutasfiri na kusimamia Sera, Sheria na Taratibu za Serikali katika kijiji.
6. Kuandaa Taarifa za Utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa, umaskini na kuongeza uzalishaji mali;
7. Kiongozi wa Wakuu wa Vitengo vya Kitaalam katika Kijiji;
8. Kusimamia, kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na Nyaraka za Kijiji;
9. Mwenyekiti wa Kikao cha Wataalamu waliopo katika Kijiji;
10. Kupokea, kusikiliza na kutatua malalamiko na migogoro ya wananchi;
11. Kusimamia utungaji wa Sheria Ndogo za Kijiji na
12. Atawajibika kwa Mtendaji wa Kata.

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji, **Nyamilangano - USHETU**, S. L. P. 50, KAHAMA, SHINYANGA.
Barua pepe: ded@ushetudc.go.tz

Tovuti: www.ushetudc.go.tz



Amul

Mshahara;

Ngazi ya Mshahara wa Serikali **TGS B.**

MASHARTI YA JUMLA

1. Mwombaji awe raia wa Tanzania na umri usiozidi miaka 45 na usiopungua miaka 18.
2. Mwombaji awe hajawahi kushitakiwa kwa kosa lolote la jinai.
3. Waombaji waambatanishe nakala za vyeti vya taaluma (NTA level 5), nakala ya cheti cha Kidato cha nne/sita vilivyothibitishwa na Hakimu au Wakili anayetambulika na Serikali.
4. Waombaji wote waambatanishe nakala ya cheti cha kuzaliwa
5. Waombaji wote waambatanishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed Curriculum Vitae) ikiwa na anuani, namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini "referees" watatu (3) na picha mbili "passport size" za hivi karibuni (ziandikwe jina kwa nyuma).
6. Testimonials, Provisional Results, Statement of Results, Hati za matokeo za kidato cha nne na sita (Form IV and VI Results Slips) na Transcript ambayo haikuambatanishwa na cheti havitakubaliwa.
7. Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vinahakikiwa na kuidhinishwa na Mamlaka husika (NECTA au NACTE).
8. Waombaji ambao tayari ni waajiriwa katika nafasi za kuingilia walioko katika Utumishi wa Umma wasiombe nafasi hizi.
9. Waombaji waliostaafishwa katika Utumishi wa Umma kwa sababu yoyote ile hawaruhusiwi kuomba nafasi hizi.
10. Waombaji watakaowasilishaji vyeti, taarifa na sifa za kughushi watachukuliwa hatua za kisheria na mamlaka zinazohusika.
11. Maombi yote yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.
12. Kwa waombaji wenye vyeti vya ngazi yaani NTA level 4, na level 6, maombi yao hayatafanyiwa kazi.
13. Mwisho wa kutuma maombi ya kazi ni siku ya Jumatatu, tarehe 30 Agosti 2020, saa 09:30 Alasiri.
14. Maombi yote yatumwe kwa njia ya posta kupitia anuani ifuatayo;

Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu,
S.L.P. 50,
KAHAMA.



Matomora M. A.
MKURUGENZI MTENDAJI.



Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji, **Nyamilangano - USHETU**, S. L. P. 50, KAHAMA, SHINYANGA.
Barua pepe: ded@ushetudc.go.tz Tovuti: www.ushetudc.go.tz

Nakala: Katibu Tawala (M),
S.L.P 320,
SHINYANGA.

Katibu Tawala (W),
S.L.P 01,
KAHAMA.

Mbao zote za Matangazo,
Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu, Msalala na Mji Kahama.
USHETU – KAHAMA.

